SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA WAATHIRIKA
**WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU** 2023

TUME YA KIMATAIFA YA **HAKI ZA BINADAMU**

JESHI LA WOKOVU

# NIMESIKIA VILIO VYAO



## MSAADA KWA VIJANA

Imeandikwa na **Meja Anugrah M. Masih**
*Teritori ya India Kaskazini*

**'Hata baada ya siku zile nyingi mfalme wa Misri akafa; wana wa Israeli kwa sababu ya ule utumwa, wakalia, kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa. Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Mungu akawaona wana wa Israeli, na Mungu akawaangalia.' (Kutoka 2:23-25).**

### UTUMWA NI NINI?

Utumwa sio wazo jipya. Ni jambo ambalo limekuwepo kwa miaka maelfu mengi na umekuwa sehemu ya jamii mbalimbali kama vile Mesopotamia, Uyunani, Rumi na Misri. Utumwa ni pale ambapo mtu humtawala mtu mwingine kama yule mtu ni kitu au ni mali yake. Utawala huo hutegemea tishio na/au matumizi halisi ya ukatili iwe wa kimwili, kihisia, kisaikolojia, kiroho au kifedha. Wakati watu wanapitia utumwa, wananyonywa. Hii maana yake ni kwamba wanatendewa isivyo halali kwa manufaa ya mtu mwingine.

Watu walio katika utumwa wanadhalilishwa na kutendewa kama wao ni kitu. Utu wao na uwezo wa kufanya maamuzi wananyang'anywa. Vikwazo vinawekwa kila sehemu ya maisha yao. Wanalazimishwa kutoa sadaka tumaini lao, ndoto zao, wapendwa wao, mambo yao ya nyuma na ya mbele. Kama wanalipwa kwa kazi zao, huwa sio kiwango cha kutosheleza kuishi. Huwanyang'anya uhuru wao na ni ukiukaji wa haki zao za binadamu.

Ni vigumu kufikiria maisha chini ya utumwa. Biblia inasema sisi sote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Watu wanaowaweka watumwa hawawatendei watu kwa heshima ambayo Mungu alitupa sisi sote. Utumwa huwanyang'anya watu uhuru wao, furaha, nafasi, tumaini na mengi mengine. Huondoa mwanga ambamo watu wote waliumbwa waishi humo na washirikishane na wengine. Badala yake huwazunguka katika giza.

Makisio ya duniani ya mwaka 2022 yanaonyesha kwamba watu wanaopitia utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu duniani imeongezeka kufikia wastani wa watu milioni 49.6 siku yoyote. Hii maana yake duniani wastani wa:

- Watu milioni 27.6 wanakabiliwa na kazi za kulazimishwa na unyonyaji wa ngono.
- Watu milioni 22 wanakabiliwa na ndoa za kulazimishwa.

## UTUMWA UNAFANANAJE KOTE DUNIANI?

**Utumwa unaweza kuwa na sura nyingi mbalimbali kote duniani. Hapa kuna mifano kadhaa:**

Angela* ni yatima anayeishi na mjomba na shangazi yake. Alipofika kuishi nao, aliambiwa kwamba kila siku, atatakiwa kusafisha nyumba, atapika vyakula vyote, atafua nguo zote na atakamilisha jukumu lolote atakalopewa. Hii ilimaanisha kwamba atakosa kwenda shule siku nyingi ili aweze kukamilisha yote.

Baba yake Klenam* alipoteza kazi yake kijijini. Familia yao ilikuwa kubwa ikiwa na watoto wengi wa kuwalisha. Wakati jirani alipomtambulisha Klenam kwa mtu alimwahidi kazi yenye malipo mazuri na nafasi ya yeye kumaliza shule, alifikiria nafasi hii itasaidia familia yake. Ni wakati alipofika huko, hakwenda shule. Badala yake, alifanya kazi masaa 12 – 14 kila siku kwenye boti ya uvuvi wa uduvi akizamia majini kukwamua nyavu huku halipwi chochote na kupata chakula kidogo kwa kazi hii ya hatari.

Familia ya Fatemeh* waliukimbia mji wao wakati wana mgambo walipovamia wakaanza kuwashambulia wale waliokuwa wanaishi hapo. Wakiwa wamehamishwa na wanaishi katika kambi ya wakimbizi, baba yake na Fatemeh alimuoza licha ya yeye kuwa bado mdogo sana huku akiwaambia familia yake kwamba hakutaka kuolewa. Sasa, mume wake ambaye ni mkubwa zaidi na mama mkwe wanatawala kila eneo la maisha yake na wananufaika na kazi anazozifanya nyumbani.

Rafiki wa kiume wa Sally ni mzuri na mchangamfu. Anampa zawadi mda wote. Anamfanya Sally ajisikie anapendwa na anakubalika. Sally amekuwa siku zote akitafuta mahali atakapopaita nyumbani na mtu ambaye atamtunza. Baada ya majuma kadhaa ya haya kufanyika, rafiki yake wa kiume akamwambia anatakiwa amlipe na amsaidie kwa kufanya tendo la ndoa na marafiki zake. Alipojaribu kukataa na kuondoka, rafiki yake huyo alikuwa katili kwake na akatishia ataiumiza familia yake Sally.

Ravi* alikuwa na umri wa miaka 12 wazazi wake walipotoa ruhusa aende na mwajiri aliyeahidi atapata mshahara mzuri kwa kutengeneza mazulia. Walipofika huko, mwajiri alimlazimisha Ravi afanye kazi kwa masaa mengi. Kile ambacho hakumaliza mchana alilazimishwa kumaliza usiku kwa mshumaa. Hakulipwa kama alivyoahidiwa, chakula hakupewa mara kwa mara na hali ya maisha yake ilikuwa mbaya.

**Jina limebadilishwa ili kumlinda.*

## FUNDISHO LA BIBLIA

Kitabu cha Kutoka ni hadithi kuhusu utumwa ambao wana wa Israeli walipitia. Sehemu hii ya hadithi, Waisraeli walikuwa wanaishi katika nchi ya kigeni – Misri. Alikuwepo Farao mpya ambaye hakufahamu lolote kuhusu Yusufu na jinsi Waisraeli walivyokuja kuishi huko. Farao huyu hakujua jinsi Yusufu alivyouzwa na kaka zake, akaletwa Misri, akashutumiwa kwa uongo na akafungwa. Hakujua lolote kuhusu mpango wa Mungu juu ya maisha ya Yusufu na akamtoa gerezani na kisha akamfanya wa pili kwa madaraka Misri. Katika wajibu huu, Yusufu aliweza kuwasaidia kaka zake wakati wa njaa na akawahamishia Misri.

Waisraeli walivyoongezeka kwa idadi na nguvu, Farao aliwaogopa. Aliwaambia watu wake: 'Haya, na tuwatendee kwa akili, wasije wakaongezeka, tena, kukitokea vita, wao nao wasije wakashikamana na adui zetu na kupigana nasi, na kutoka katika nchi hii.' (Kutoka 1:10). Kwa hiyo Farao akawafanya Waisraeli wawe watumwa. Aliweka wasimamizi wa kazi juu yao na

akawanyonya kwa kazi zao. Walikandamizwa na Wamisri waliokuwa hawana huruma kwa kuwapa kazi. Maisha yao yalifanywa kuwa machungu na yasiyovumilika kwa kujenga miji ya Pithomu na Ramesesi (Kutoka 1:11-14). Zaidi sana hata ikafanya ' Waisraeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia'(Kutoka 2:23).

Kwa shukrani, tunafahamu kwamba Mungu aliwajali Waisraeli na kwamba walikuwa na thamani mbele zake. Aliwapenda sana na alisikia vilio vyao vya huzuni. Tunasoma katika Kutoka 2:23-25 kwamba, 'kilio chao kikafika juu kwa Mungu: Mungu akasikia kuugua kwao. Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Mungu akawaona wana wa Israeli, na Mungu akawaangalia.'

## MASWALI YA KUJADILIANA

**Vifungu hivi vinasema nini kumhusu Mungu? Vinasema yeye hufanya nini?**

Miaka yote hii maelfu iliyopita wakati wana wa Israeli walikuwa wanatendewa vibaya kama watumwa, Mungu alijali sana kuhusu hali yao. Sio tu alisikia vilio vyao na kuugua kwao, lakini alisikiliza. Aliona kilichokuwa kinaendelea. Akakumbuka agano lake na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Mungu alisukumwa kufanya kitu tunapoona hadithi ya Kutoka ikijifunua. Mungu alipoanza kuwaondoa watu wake watoke utumwani na giza lake waende katika mwanga wake.

Katika dunia leo, Mungu bado anajali vile vile kuhusu mamilioni ya watu walio utumwani – watu wazima na watoto. Anasikia na anawasikiliza akina Angela, Klenam, Fatemeh, Sally na akina Ravi wa dunia hii, ambao wanatendewa visivyo na wanaoshangaa kama yupo yeyote anayewajali. Vifungu hivi kutoka Kutoka vinatufahamisha kwamba hawako peke yao, na kwamba Mungu anasikia, Mungu anaona naye anaelewa.

Mungu vile vile anatutaka sisi tuwajali wale ambao wamo utumwani na wamenaswa katika utumwa. Anatutaka tufahamu kwamba kuna njia za kuwasaidia watu wanaopitia katika utumwa.

## MASWALI YA KUJADILIANA

**Una mawazo yoyote ya namna gani mnaweza kukomesha utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu mahali ulipo?**

Baadhi ya mambo mnayoweza kufanya ni:

1. Fahamu ishara – jifunze ufahamu ni viashiria gani vinavyoweza kukuonyesha mtu fulani ananyanyaswa. Kuna mambo mengi ya kuangalia, ikiwa ni pamoja na hali za maisha ya watu, hali za kufanya kazi na kugundua jinsi watu wazima wanaowazunguka wanavyowatendea.

2. Jifunze namna ya kuwa salama mitandaoni – wewe na marafiki zako mnaweza kutunzana namna gani ili muwe salama?

3. Waambie wengine (tetea) – mara unapotambua ishara, washirikishe wengine ili na wao wafahamu vile vile. Washirikishe wana familia na marafiki zako ulichojifunza leo na viashiria vya utumwa. Hii husaidia kujenga jamii zilizo salama. Tafuta ujue kama mahali unapoishi kuna misaada kwa wanusurika. Sehemu nyingine, kama unashuku kwamba mtu fulani anaweza kuwa yumo utumwani, unaweza kutoa ripoti. Fanya kazi na kundi dogo katika jamii yako kuongeza/kusambaza ufahamu wa swala hili. Labda unaweza kufanya jambo shuleni kwako, sehemu yako ya kazi au kanisani kwako?

4. Jifunze zaidi kuhusu utumwa, usafirishaji haramu wa binadamu na unyonyaji. Ishirikishe familia yako, marafiki zako na familia ya kanisa lako. Fanya uwasilishaji shuleni kwako, sehemu yako ya kazi au kanisani kwako.

5. Omba! Waombee watu ambao wanapitia utumwa Mungu awalinde na asikie maombi yao. Waombee viongozi wetu na mashirika yanayowasaidia wanusurika.

6. Watendee watu kwa wema, heshima na upendo.

7. Wahimize marafiki zako na wana familia yako wawatendee watu kwa heshima, wema na upendo.

8. Waulize viongozi shuleni kwako au kanisani na hata serikalini wawalinde na kuwasaidia vizuri zaidi watu ambao hawako salama.

---

Hebu tuombe pamoja kwa ajili ya wale wote duniani walio utumwani na wanaotendewa kama watumwa.

Mpendwa Yesu,

Tafadhali wasaidie watumwa wote na wale walio utumwani duniani. Linda mioyo yao na akili zao. Wawezeshe wapate uhuru na wasaidie wapate usalama. Linda familia zao na saidia familia ambazo zimetengwa ziweze kurudiana tena. Wasaidie wafahamu unawapenda na unawajali na kwamba upo pamoja nao hata kama maisha ni magumu na yana huzuni. Wawezeshe wafahamu wao ni wa muhimu na wanapendwa.

Amina

Maombi kutoka kwa Alina, mwenye umri wa miaka 9 – yaliyotolewa kwa kibali ndani ya mfumo wa maadili ya utoaji hadithi.

## SHUGHULI

KITUO CHA MAOMBI